Halmashauri tengeni fedha za mapato ya ndani na kujenga mabweni kwani mnao uwezo

Muleba, mkoani Kagera alisema katika kukabili changamoto ya ajira kwa vijana,



Sanga).

HABARI LEO UK 8.

# Wafugaji kusaidiwa masoko na programu za simu, SMS

**Na Mwandishi Maalumu, Hyderbad**

IMEELEZWA kuwa matumizi ya programu za simu na huduma za ujumbe mfupi ili kusambaza taarifa za soko kwa wakulima na wafugaji kutawezesha kufanyika kwa maamuzi sahihi kuhusu lini, wapi na nini cha kuuza sokoni.

Kauli hiyo imetolewa na Daktari wa Mifugo wa Halmashauri ya Chamwino, Dk David Msimbe wakati akifanya wasilisho katika mafunzo yaliyoshirikisha nchi 13 ikiwamo Tanzania jijini Hyderbad, India.

Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Indian Technical and Economic Cooperation(ITEC) na kufanyika katka Taasisi ya Agricultural Extension Management (MANAGE) jijini Hyderbad, India.

Akizungumzia mnyororo wa utumiaji wa mfumo wa ugavi na upatikanaji wa soko nchini alisema mawasiliano hayo yataondoa changamoto zinazojitokeza katika kung'amua hali halisi ya soko.

Alisema kutokana na wakulima wengi wa Tanzania kuwa na uwezo mdogo wa kufikia masoko rasmi kuwapo kwa mawasiliano ya simu na ujumbe mfupi kutafungua ukubwa wa soko.

"Mara nyingi wakulima na wafugaji wetu hutegemea masoko ya ndani yasiyo rasmi, ambapo bei ni ya chini na taarifa za soko ni chache, lakini kwa kutumia mawasiliano fursa nyingi za soko zitaonekana," alisema.

Aidha alisema mfumo huo unaweza kuchukua jukumu muhimu katika kutatua changamoto zinazokabili sekta ya kilimo na ufugaji na kuboresha fursa zake.

"Tunaweza kufanikisha hili kwa kukuza ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)," alisema.

Aidha alisema kwa kuwa tayari Tanzania inashirikiana na sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya ugavi, kama vile maghala, usafirishaji na soko, ufikiaji wa huduma za kifedha na uwekezaji kidijiti utaimarisha soko.

Akizungumzia maendeleo ya miundombinu, Dk Msimbe alisema uwekezaji unaoendelea kufanywa katika mitandao ya barabara za vijijini na miundombinu ya usafirishaji itapunguza gharama za usafirishaji na kuwawezesha wakulima na wafugaji kufikia masoko kwa urahisi zaidi.

"Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuuza nje, hasa kwa mazao ya thamani ya juu kama vile kilimo cha bustani, viungo na kahawa. Miundombinu iliyoboreshwa ya ugavi na uzingatiaji wa viwango vya ubora hufungua masoko ya kimataifa," alisisitiza.

Aidha aliwaeleza washiriki wa mafunzo hayo kuwa Serikali ya Tanzania imeweka bayana ajenda na vipaumbele vya kilimo na mifugo katika mikakati ya miaka mingi na ya kisekta ukiwemo Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III), Pathways for Sustainable Food Systems 2030 na Ajenda 10/30 (ADBG,2023).

